

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"
Telephone: + 028 2750271
Fax: + 028 2750376
E-mail: ded@maswadc.go.tz
Kumb. Na. CADM/5/13/Vol.II/98



S.L.P 170,
MASWA,
SIMIYU.

21.8.2017

TANGAZO LA KAZI YA MKATABA

(MARUDIO)

Mkurugenzi Mtendaji (w) Maswa anawatangazia wananchi wote wenye sifa nafasi 2 za kazi ya mkataba ya msaidizi wa hesabu (Accounts Assistant).

A: SIFA ZA MWOMBAJI :

1. Awe amemaliza kidato cha IV au VI
2. Awe na cheti cha atec level II au "Foundation Level" kinachotolewa na NBAA au cheti cha Uhasibu (Certificate in Accountancy)
3. Awe na umri usiozidi miaka 45

B: KAZI ZA KUFANYA

Kusimamia fedha zote zinazohusu huduma za Afya zitakazotolewa na Serikali na Wadau wa Maendeleo katika Vituo vya Afya na Zahanati.

C: MUDA WA MKATABA

Mkataba utakuwa wa mwaka mmoja mmoja kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018 na utazingatia utendaji kazi na kipindi ambacho Wafadhili watagharamia ajira hizo.

D: MSHAHARA

Mshahara utakuwa ngazi ya TGS B sawa na sh.390,000/= kwa mwezi ambao utatolewa na Wafadhili.

E: JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua za Maombi zitumwe kwa:
Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
S.L.P 170,
Maswa – SIMIYU

Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma na Cheti za kuzaliwa. Watakaoitwa kwenye usaili wafike na vyeti halisi (Original certificates). Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/09/2017 saa 9.30 alisiri.



Dr. Sagamiko F.D.
Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya
MASWA